

Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (kulia) akikabidhiwa nyaraka za ofisi na Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa benki hiyo, Japhet Justine katika ofisi za benki hiyo, Dar es Salaam jana. (Na Mpigapicha Wetu).

# Ulega ataka tafiti ziwafikie wafugaji

**Na Hamisi Kibari**

**N**AIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewataka watafiti wa mifugo kuhakikisha tafiti zao zinakwenda hadi kwa mfugaji wa chini ili kumsaidia kubadilisha maisha yake na siyo kusomwa kwenye makongamano.

Pia amewataka watafiti na wadau wengine wa mifugo kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima ili wabadilike na kuanza kupanda malisho kwa ajili ya mifugo yao na kukazania dhana ya ufugaji kibiashara.

Ulega alitoa wito huo jana Dar es Salaam wakati akifungua mkutano kuhusu

mazungumzo ya hatua za kisera katika uzalishaji wa maziwa unaozingatia weledi na mabadiliko ya tabianchi.

Moja ya malengo ya mazungumzo hayo ni kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa kufanya mabadiliko ya sekta ya mifugo ili iwe ya kisasa na kuendeshwa kwa weledi zaidi.

“Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga kuona kilimo, ufugaji na uvuvi mbali ya kutoa ajira, vinachangia zaidi katika Pato la Taifa,” alisema Ulega.

Alisema kumekuwa na tatizo la watafiti kushindwa kutoa suluhisho kwa mwananchi mmoja mmoja na kutoa matokeo chanya kwa jamii.

Kuhusu malisho, Naibu

Waziri huyo alisema kuna tatizo kubwa la wafugaji kutoamini wanaweza kupata mafanikio makubwa zaidi kwa kulima malisho ya mifugo yao wenyewe.

Alisema takwimu zinaonekana ng’ombe wa asili hutoa kati ya lita 1.5 mpaka tatu kwa siku, wakati inatakiwa mara tatu au zaidi ya hapo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (Taliri), Profesa Erick Komba alisema katika tafiti zao wamegundua ufugaji wa ng’ombe nchini licha ya kuwa na tija ndogo, pia unachangia kuzalisha hewa ukaa inayosababisha joto kuongezeka na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mambo mawili yanaweza kulitoa taifa mahala

hapo ambayo ni kuja na mbari bora na wafugaji kupanda au kutumia malisho yenye virutubisho muhimu kwa mifugo.

Alisema kukiwa na ufugaji bora, ng’ombe watakuwa wachache lakini wakitoo maziwa mengi na hawatatoa kaboni nyingi inayotokana na mmeng’enywa wa chakula pamoja na samadi wanayotoa na kuchangia ongezeko la joto duniani.

Mkurugenzi wa Tafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Angello Mwilawa alisema Tanzania inahitaji kujielekeza zaidi katika mafunzo na huduma za ugani ili kuwajengea uwezo wafugaji kuzalisha malisho bora na utunzaji wake.